
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA
UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

# IKISIRI YA SHERIA YA SERIKALI MTANDAO 2019



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI
WA UMMA NA UTAWALA BORA

## Mamlaka ya Serikali Mtandao

# IKISIRI YA SHERIA YA SERIKALI MTANDAO 2019

# MAWASILIANO NA MAMLAKA

## MAKAO MAKUU

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa
Umma na Utawala Bora
Mamlaka ya Serikali Mtandao,
Mtumba-Mtaa wa Mtandao
S.L.P 2833, Dodoma
Baruapepe: info@ega.go.tz
Tovuti: www.ega.go.tz

## DAR ES SALAAM

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa
Umma na Utawala Bora,
Mamlaka ya Serikali Mtandao
8 Barabara ya Kivukoni, Jengo la Utumishi
S.L.P 4273, Dar es Salaam
Baruapepe: info@ega.go.tz
Tovuti: www.ega.go.tz

## KITUO CHA UTAFITI NA UBUNIFU

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa
Umma na Utawala Bora,
Mamlaka ya Serikali Mtandao, Jengo la Zamani la
Maabara ya Kompyuta, Ndaki ya Sayansi ya Kompyuta,
Habari na Mawasiliano (CIVE),
Chuo Kikuu cha Dodoma.
S.L.P. 2833, 40404 Dodoma

# YALIYOMO

**UTANGULIZI** .......... 1
Dhana ya Serikali Mtandao .......... 1
Historia Fupi .......... 1
Dira .......... 2
Dhamira .......... 2
Misingi Mikuu .......... 2
Uadilifu .......... 2
Ubunifu .......... 2
Kuthamini Wateja .......... 3
Kufanyakazi kwa Pamoja .......... 3
Ushirikiano .......... 3
Weledi .......... 3

**SHERIA YA SERIKALI MTANDAO NA. 10 YA MWAKA 2019** .......... 4

# UTANGULIZI

## Dhana ya Serikali Mtandao

Serikali mtandao au Serikali Kidijitali ni matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utendaji kazi Serikalini kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuboresha utoaji wa huduma kwa umma kwa urahisi, haraka na gharama nafuu.

## Historia Fupi

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ni taasisi ya umma iliyorithi iliyokuwa Wakala ya Serikali Mtandao ambayo ilianzishwa Aprili, 2012 kwa Sheria Na. 30 ya Wakala za Serikali, Sura ya 245 ya Mwaka 1997. Wakala hii ilikuwa na jukumu la kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao nchini.

Aidha, Mamlaka ya Serikali Mtandao ilianzishwa mwaka 2020 kwa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019 kwa lengo la kusimamia, kuratibu, kuendeleza na kukuza jitihada za Serikali Mtandao pamoja na kuhimiza uzingatiwaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa taasisi za umma. Mamlaka hii iliongezewa nguvu ya usimamizi na udhibiti wa utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao kwa taasisi za umma.

Mamlaka ya Serikali Mtandao ilianza kazi rasmi kutokana na tangazo la Serikali Na. 75/2020 la tarehe 7 Februari, 2020, ambalo liliifuta rasmi iliyokuwa Wakala ya Serikali Mtandao na Mamlaka kurithi majukumu, kazi na afua zote za iliyokuwa Wakala ya Serikali Mtandao.

## Dira
Kutambuliwa kuwa taasisi inayoongoza kwa ubunifu katika kuwezesha matumizi ya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha utoaji huduma kwa umma.

## Dhamira
Kujenga mazingira wezeshi ya kisheria kwa ajili ya uratibu, usimamiaji na uendelezaji wa matumizi ya TEHAMA ili kuboresha utoaji wa huduma za Serikali kwa umma.

## Misingi Mikuu
Mamlaka inaongozwa na misingi mikuu Sita ambayo inaelekeza kuhusu tabia na mwenendo wa watumishi wake kwa ngazi zote. Misingi hiyo inafafanua utamaduni wa mahali pa kazi, kuhakikisha watumishi wote na wateja wa Mamlaka wana uelewa wa pamoja wa jinsi wanavyotakiwa kuhudumiwa na nini kichotarajiwa kutoka kwao.

## Uadilifu
Tunafuata viwango vya uendeshaji vya hali ya juu katika kila tunachofanya kwa kutambua kuwa uhusiano wa kweli na uaminifu ni muhimu kwa mafanikio endelevu ya taasisi.

## Ubunifu
Tunazingatia utamaduni wa Mamlaka unaothamini uasili wa uvumbuzi na ubunifu katika kukuza vipaji kwa kuzingatia uwazi na ari.

## Kuthamini Wateja

Tunajitoa kwa dhati kuwasaidia wateja wetu wa nje kutimiza malengo yao kwa kuelewa shughuli wanazofanya na kuwapa kile wanachokithamini zaidi.

## Kufanyakazi kwa Pamoja

Tumedhamiria kufanya kazi kwa pamoja tukiwa na mawasiliano sahihi ili kufikia malengo yaliyowekwa.

## Ushirikiano

Tunafanya kazi kwa uwazi na taasisi za umma na wadau wengine huku tukibadilishana taarifa, maarifa, uzoefu na tukitambua kuwa tunategemeana kwa maendeleo ya Serikali mtandao.

## Weledi

Tunazingatia ubora wa kazi kwa kiwango cha juu na kutoa huduma bora kwa wateja wetu

# SHERIA YA SERIKALI MTANDAO NA. 10 YA MWAKA 2019

1. **Je, Mamlaka ya Serikali Mtandao inaogozwa na nani?**

   Mamlaka inaongozwa na Bodi ya Wakurugenzi kwa kushirikiana na Mkurugenzi Mkuu kwa kuzingatia majukumu kama yalivyoainishwa katika Sheria.

2. **Mamlaka ya Serikali Mtandao ina majukumu na kazi gani?**

   a) Kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango, Taratibu na Miongozo ya Serikali Mtandao.

   b) Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa taasisi za umma kuhusu utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao.

   c) Kufanya ukaguzi na tathmini ya usalama wa mifumo ya TEHAMA Serikalini na mifumo ya taasisi binafsi inayotoa huduma kwa Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine husika.

   d) Kupitia, kuboresha na kuidhinisha miradi ya TEHAMA ya taasisi za umma kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa.

   e) Kuwezesha taasisi za umma kupata miundombinu na mifumo ya TEHAMA ya pamoja.

f) Kukuza utafiti na ubunifu katika uendelezaji wa Serikali Mtandao katika taasisi za umma;

g) Kutoa miongozo, ushauri na msaada wa kufundi katika utekelezaji wa jitihada za Serikali mtandao kwa taasisi za umma.

## 3. Nini madhumuni ya Sheria ya Serikali Mtandao?

Madhumuni ya Sheria ya Serikali Mtandao ni kuweka masharti ya huduma za Serikali mtandao; kuanzisha Mamlaka ya Serikali mtandao na usimamizi wake; usimamizi na uendeshaji wa huduma za Serikali-mtandao; usimamizi wa taarifa za kielektroni.

## 4. Je, muundo wa usimamizi wa Serikali Mtandao umegawanyika katika ngazi ngapi?

Muundo wa Serikali Mtandao umegawanyika katika ngazi kuu tatu ambazo ni:

a) Kamati ya Kitaifa ya Uongozi ya Serikali Mtandao ina jukumu la kutoa miongozo ya kimkakati na kisera kuhusu utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao.

b) Kamati ya Kitaalamu ya Serikali Mtandao ina jukumu la kuishauri Kamati ya Kitaifa ya Uongozi kuhusu masuala ya Serikali Mtandao na kutekeleza majukumu mengine kama itakavyoelekezwa na Mamlaka au Kamati ya Kitaifa ya Uongozi.

c) Kamati ya Kitaasisi ya Uongozi ya Serikali Mtandao

ina jukumu la kuainisha maeneo ya vipaumbele yanayohitaji kutumia TEHAMA kwa muktadha wa kuanzishwa kwa taasisi husika, kusimamia uendeshaji na usalama wa TEHAMA kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao. Kamati hii ni ya lazima kwa kila taasisi ya umma kwa mujibu wa Sheria na Mwenyekiti wake ni Afisa Masuuli wa taasisi husika ambapo Katibu ni Mkurugenzi au Mkuu wa Idara au Kitengo cha TEHAMA.

5. **Je, kamati hizi zinatakiwa kufanya vikao vyake mara ngapi kwa mwaka wa fedha?**

Kamati hizi zinatakiwa kufanya vikao vyake mara 4 kwa mwaka ikiwa ni mara moja kwa kila robo ya mwaka au wakati wowote endapo kutakuwa na uhitaji wa lazima.

6. **Je, wajumbe wa kamati hizi ni akina nani?**

Wajumbe wa kamati wameainishwa katika Sheria kwenye vifungu namba 16, 17 na 18 hata hivyo kamati zinaweza wakati wa mkutano, kumualika mtaalamu yeyote iwapo kuna jambo linalohitaji ufafanuzi.

7. **Je, Kitengo cha TEHAMA kwa taasisi za umma kimeundwa kwa mujibu wa Sheria?**

Sheria inaanzisha Kitengo cha Usimamizi wa TEHAMA katika taasisi zote za umma na kuwataka Maafisa Masuuli kuajili watumishi wenye weledi na umahili kulingana na ukubwa wa matumizi ya TEHAMA katika Taasisi.

8. **Nini wajibu wa taasisi za umma katika ujenzi wa miundombinu?**

Sheria inazitaka taasisi za umma kuhakikisha ujenzi wa miundombinu ya Serikali kama vile barabara, reli na majengo ya Serikali yanAkuwa na utayari wa kuunganishwa na miundombinu na mifumo ya TEHAMA.

9. **Nini wajibu wa taasisi za umma katika kupanga, kutekeleza na kuendeleza miradi ya TEHAMA?**

Kila taasisi ya umma inatakiwa kutoa taarifa ya uanzishwaji wa mradi wa TEHAMA kwa Mamlaka kwa ajili ya kupata ushauri na idhini. Aidha, baada ya kupata idhini taasisi itaendelea kutoa taarifa ya uendelezaji kwa hatua zote kupitia Mfumo wa Huduma za TEHAMA Serikalini (Government ICT Services Portal-GISP) unaopatikana kwa anuani ya https://gisp.gov.go.tz/

10. **Je, Mamlaka ya Serikali Mtandao inauwezo wa kudai taarifa za mifumo au miundombinu ya TEHAMA kutoka kwa taasisi za umma?**

Mamlaka ya Serikali Mtandao chini ya Sheria hii imepewa mamlaka ya kudai taarifa yoyote, nyaraka, rekodi au ripoti kuhusu mifumo au miundombinu ya TEHAMA kutoka kwa taasisi yoyote ya umma. Pia, inaweza kufanya uchunguzi au ukaguzi wa utendaji wa mradi, mifumo au miundombinu ya TEHAMA katika taasisi za umma.

11. **Iwapo taasisi ya umma itatekeleza mradi wa TEHAMA bila kushirikisha Mamlaka ni hatua gani zinaweza kuchukuliwa?**

Mamlaka inaweza kusimamisha utekelezaji wa mradi wowote wa TEHAMA unaotekelezwa na taasisi ya umma ambao haujazingatia Sheria, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao kwa maslahi ya taifa.

12. **Ni mambo gani ya kuzingatia wakati taasisi ya umma inataka kuanzisha mifumo ya TEHAMA?**

Taasisi ya umma inatakiwa kuanishisha mahitaji ya mfumo, kushirikisha wadau kuepuka urudufu, kuangalia uwezo wa wataalamu wa ndani ya taasisi au Serikalini kwa ajili ya kusanifu na kutengeneza mfumo huo.

13. **Je, mifumo yote ya TEHAMA inayotumiwa na Serikali lazima ijengwe na Serikali pekee?**

*Hapana!* Mifumo ya TEHAMA inayotumiwa na Serikali sio lazima kujengwa na Serikali pekee. Sekta binafsi pia ina nafasi kubwa ya kujenga mifumo ya TEHAMA kwa taasisi za umma kutokana na mahitaji ya taasisi hizo. Jambo muhimu ni kuzingatia matakwa ya Sheria ya Serikali Mtandao, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao inayopatikana katika tovuti ya eGA kwa anuani ya www.ega.go.tz.

14. **Je, taasisi ya umma inatakiwa kuhifadhi wapi mifumo yake ya TEHAMA?**

Sheria ya Serikali Mtandao inazitaka taasisi za umma kuhifadhi mifumo yake ya TEHAMA katika miundombinu iliyoidhinishwa na Serikali.

15. **Kwa nini Sheria inasisitiza taasisi za umma kutumia mifumo na miundombinu shirikishi ya TEHAMA?**

Sheria inasisitiza taasisi za umma kutumia mifumo na miundombinu shirikishi ya TEHAMA ili kuepuka uwepo wa mifumo mingi inayofanya kazi zinazofanana na kupunguza gharama za uendeshaji.

16. **Je, ni taasisi zipi za umma ambazo hazilipi ada na tozo za matumizi ya mifumo Shirikishi ya TEHAMA?**

Taasisi za umma ambazo zimesamehewa kulipa ada na tozo za matumizi ya mifumo Shirikishi ya TEHAMA ya Baruapepe Serikalini (GMS), Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office) na Mfumo wa Kusimamia Shughuli na Rasilimali za Taasisi (ERMS) ni Wizara, Idara Zinazojitegemea (Zilizoorodheshwa katika Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma), Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

17. **Je, sheria inatambua uwepo wa jukwaa la kuwasiliana na kubadilishana taarifa Serikalini kwa njia ya kielektroni?**

Sheria inatambua uwepo wa mfumo ambao ni jukwaa la

kuwasiliana na kubadilishana taarifa kwa lengo la kuongeza ufanisi na utoaji uamuzi na huduma kwa umma.

18. **Je, taasisi za umma zitakiwa kufanya nini ili kutoa huduma za Serikali kwa njia ya kieletroni?**

Sheria inazitaka taasisi za umma kuboresha taratibu zake za kiutendaji kutoka zilizozoeleka (Manual work) kwenda kielektroni na kupunguza matumizi ya karatasi kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao ili kutoa huduma kwa urahisi, haraka na kwa gharama nafuu.

19. **Je, Sheria inatambua shughuli zinazofanywa na Serikali Kielektroni?**

Ndiyo, Sheria inatambua shughuli zinazofanywa na Serikali kielektroni ambazo zinajumuisha kutoa huduma kielektroni, kuwasilisha taarifa, data, habari na nyaraka kupitia njia zilizoidhinishwa.

20. **Je, usalama wa Serikali Mtandao ni nini?**

Usalama wa Serikali Mtandao ni kitendo cha kuilinda miundombinu ya kimtandao na vifaa vya kimtandao kama kompyuta, simu, mifumo ya TEHAMA pamoja na taarifa zilizomo dhidi ya mashambulizi ya kimtandao.

21. **Je, kuna usalama wa huduma zinazotolewa na Serikali kwa njia mtandao?**

Ndiyo, usalama upo kwa kuwa Serikali kupitia Mamlaka ya

Serikali Mtandao na kwa mujibu wa Sheria ina kituo mahususi cha uendeshaji wa usalama wa Serikali Mtandao kinachofanya kazi kwa saa 24 kwa siku 7 za wiki.

22. **Nini wajibu wa taasisi za umma kwenye suala ya usalama wa Serikali Mtandao?**

Taasisi za umma zinawajibu wa kufanya tathimini ya mifumo ya TEHAMA mara kwa mara ili kubaini matishio na kutoa taarifa kwa Mamlaka. Pia, kuainisha watumiaji wa mfumo kwa kutoa utambulisho na majukumu yao katika mfumo.

23. **Sheria imezingatiaje usimamizi wa matukio ya usalama wa TEHAMA?**

Taasisi ya umma kwa madhumuni ya usimamizi wa matukio ya usalama wa TEHAMA, itabaini, kusimamia na kuwa na mikakati thabiti ya kurudisha huduma katika hali ya kawaida iwapo kutakuwa na matukio yanayohusiana na usalama wa TEHAMA na kutoa taarifa kwa Mamlaka.

24. **Nini wajibu wa taasisi za umma katika kulinda mifumo na miundombinu ya TEHAMA?**

Taasisi za umma zinatakiwa kuwa na mkakati endelevu wa usalama wa taarifa, mazingira salama na vituo mbadala vya kuhifadhi mifumo ya TEHAMA na kufanya uchunguzi makini wa watumishi ili kuhakikisha usalama wa mifumo ya TEHAMA unakuwa wa hali ya juu.

25. **Je, ni hatua gani atakayochuliwa mtumishi wa umma iwapo atakiuka masharti ya Sheria hii?**

Mtumishi wa Umma atakayekiuka masharti ya Sheria hii atachuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma au sheria nyingine husika.

26. **Je, ni makosa gani ya jinai yanayoanzishwa na Sheria ya Serikali Mtandao?**

- Kufichua au kutoa taarifa isivyo halali ambayo mtumishi ameipata kutokana na ajira yake kwa njia ya kielektroni;
- Kupakua programu zisizoruhusiwa kwa kutumia vifaa au miundombinu ya TEHAMA ya Serikali;
- Kutangaza au kusambaza habari zisizo rasmi au taarifa kupitia mifumo au miundombinu ya Serikali;
- Kuharibu taarifa au kuondoa kumbukumbu yoyote kutoka katika miundombinu ya TEHAMA ya Serikali isivyo halali.
- Kwa kujua au kwa uzembe kushindwa kuzingatia viwango na miongozo ilivyoainishwa kuhusu masuala ya usalama wa TEHAMA.
- Kushindwa kutekeleza matakwa ya kifungu cha 24 cha Sheria ya Serikali Mtandao kuhusu utekelezaji wa miradi ya TEHAMA.

27. **Je, Sheria imeainisha adhabu kwa mtumishi atakayetenda makosa yaliyotajwa hapo juu?**

Ndiyo, Sheria imeainisha kuwa mtumishi atakayetenda makosa tajwa hapo juu atahukumiwa kifungo jela au kulipa faini au vyote kwa pamoja kulingana na uzito wa kosa.




**MAKAO MAKUU**

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora
Mamlaka ya Serikali Mtandao,
Mtumba-Mtaa wa Mtandao
S.L.P 2833, Dodoma
Baruapepe: info@ega.go.tz
Tovuti: www.ega.go.tz